

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI



MAMLAKA YA UDHIBITI WA  
HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI  
(EWURA)



**TAARIFA KWA UMMA**

Katika siku za hivi karibuni, kumekuwapo na matukio ya milipuko ya moto yanayotokana na kuhifadhi ama kuuza mafuta ya petroli kwa kutumia madumu na chupa za *plastiki*, kinyume na tahadhari ya Usalama wa Afya, Mali na Mazingira (HSE).

Kwa mujibu wa Kanuni Namba 27 ya Kanuni zinazosimamia biashara ya vituo vya mafuta za mwaka 2022 kama ilivyochapishwa katika Gazeti la Serikali Na.150, wamiliki wote wa vituo vya mafuta wanatakiwa kuchukua tahadhari kwa kuhakikisha kuwa Usalama wa Afya, Mali na Mazingira (HSE) unazingatiwa ili kuepusha milipuko ya moto.

Hivyo basi, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inawakumbusha wamiliki wote wa vituo vya mafuta kuzingatia matakwa ya Kanuni Namba 27 kwa kutoruhusu uuzwaji wa mafuta ya petroli kwenye vifaa visivyoruhusiwa kuchukulia/kuhifadhia mafuta kama vile madumu, chupa za aina zote na vifaa vingine visivyoruhusiwa kisheria.

Aidha, EWURA inatoa tahadhari kwamba wakaguzi wake watafanya ukaguzi ili kubaini kama Kanuni Namba 27 inazingatiwa ipasavyo; na atakayekiuka Agizo hili atachukuliwa hatua kali kwa mujibu wa Sheria, ikiwamo kukifungia kituo husika.

**Imetolewa na  
Mkurugenzi Mkuu  
EWURA  
16/9/2024**